# HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

Nambazasimu: ShuleyaSekondariChangarawe,
MKUU WA SHULE: 0757037153 S.L.P 126, Mafinga.
M/Mkuuwashule: 0765960220/0620420409
Matroni /Patron: 0753639768/0754391778/0758217799
Ofisiyamalezi : 0754241254

Tarehe ……………………………

**MWANAFUNZI**

**……………………………………………………………………………..**

**…………………………………………………………………………….**

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHATANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE – ILIYOKO HALMASHAURI YA MJI MAFINGA MKOA WA IRINGA 2022</u>**

**1.0 UTANGULIZI**

- Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 Tahasusi ya……………………………………………………
- Shule ya sekondari Changarawe ipo umbali wa kilometa nne (04) kutoka STAND KUU ya mabasi ya Mafinga mjini barabara iendayo Mbeya.
  Usafiri wa kukufikisha shuleni ni TEKSI AU BAJAJI (SEMA UPELEKWE CHANGARAWE SEKONDARI) Nauli ya taksi ni 5,000/=, bajaji ni 3,000/= na pikipiki ni 2,000/=.
- Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe………………………………..
  Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………………………………………..
- NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI YEYOTE KUMILIKI **SIMU** YA MKONONI SHULENI
- MUDA WA MWISHO KURIPOTI SHULENI NI SAA **12:00** KAMILI ZAIDI YA HAPO HAUTOPOKELEWA KABISA HIVYO ZINGATIA MUDA.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**SARE ZA SHULE - WAVULANA**

- Suruali mbili (02) kitambaa AMERICAN KHAKI zilizoshonwa kwa heshima. Marufuku mshono wa JEANS AU MLEGEZO, AU suruali inayobana (kitambaa kimeambatanishwa).
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu yasiyo angaza.
- Koti American Khaki lililoshonwa kwa Heshima ili kufanya suti.
  (Tunashauri ushonewe sare za shule kwa mafundi wa hapa Mafinga kuepuka kuchanganya rangi / Kitambaa).
- Tai iliyoshonwa kwa Heshima ya kitambaa cheusi bila maua
- Viatu vya ngozi jozi mbili (02) rangi nyeusi vya kamba, Boots na viatu vya kuchomekea haviruhusiwi kabisa.
- Soksi jozi mbili (02) rangi nyeusi.
- Mkanda wa suruali – rangi nyeusi (usio na urembo)

- Nguo za kushindia (shamba dress) suruali mbili (2) za dark blue na t-shirt mbili za kijivu zisizo na maua (zenye kola)
- Jaketi jeusi na sweta nyeusi nguo zingine haziruhusiwi.
- Truck suit ya blue pea moja
- Jezi ya michezo ya bluu (bukta na tishirt)
- Raba za michezo / viatu vya michezo
- Nguo zingine haziruhusiwi kabisa.

**WASICHANA**

1. Sketi za rangi ya American Khaki mbili rinda boksi ndefu kufika chini, makoti mawili (ya kitambaa cha sketi) ili kufanya suti. Kitambaa kimeambatanishwa. Pia tunashauri ushonewe kwa mafundi wa hapa Mafinga kuepuka kuchanganya rangi na kitambaa.
2. Rangi ya hijab(kijuba) iwe nyeupe isiyo na urembo kwa wanafunzi wa kiislamu
3. Mashati meupe mikono mirefu mawili (2) pamoja na tai nyeusi bila maua
4. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili.
5. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
6. Truck suit ya blue Na mwanafunzi wa Kiislamu anaruhusiwa kuja na short kanzu nyeupe.
7. Nguo za kushindia (shamba dress) sketimbili (2) dark blue na T-shirt 02 rangi ya kijivu (zenye kola)
8. Jaketi jeusi na sweta nyeusi
9. Jezi ya michezo ya blue (bukta na tishirt).
10. Nguo nyingine haziruhusiwi kabisa.

**ADA NA MICHANGO YA SHULE**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule CHANGARAWE SEKONDARI 60201200061 katika Benk ya NMB.

**b) Michango mingine ni kama ifuatavyo:-**

i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv) Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
v) Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima mock
vi) Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)
vii) Mchango 10,000/=Kwa ajili ya dawa ya huduma ya kwanza shuleni.

viii) Shilingi 50,000/=Kwa ajili ya mitihani ya pamoja ngazi ya Mkoa.
NB: mwanafunzi akilazimika kupata matibabu zaidi kwenye Hospitali nyingine gharama zote za matibabu zinagharamiwa na mzazi hivyo mzazi hakikisha unamkatia motto Bima ya Afya kuepuka gharama zaidi.

- Michango yote isipokuwa ada ilipwe kwenye akaunti ya shule – changarawe sekondari – 60202300483 NMB.
- **MWANAFUNZI ASIYEKAMILISHA MICHANGO HATAPOKELEWA.**

**NB:FEDHA TASLIMU HAZITAPOKELEWA KABISA MWANAFUNZI AJE NA KARATASI YA MALIPO YA BENKI**

**c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i) Ream ya karatasi 01 (A4 photocopy paper)Kwa kila muhula
ii) Godoro la futi 2 ½ kwa futi 6.
iii) Mashuka pea 2 rangi ya pink, blanketi 1 nzito, mto 1 Na foronya 2rangi ya pinki
iv) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
v) Ndoo 2 zenye mfuniko, ujazo wa lita kumi (10)
vi) **MCHEPUO WA HGK**: jembe 1, kwanja 1na fagio 01 lainiyandani
vii) **MCHEPUO WA HGL**: jembe1, kwanja 1na fagio 01 Ngumu (brush)
viii) Kanda mbili jozi moja
ix) Kila mzazi/mlezi unaombwa kumpa fedha ya matumizi yake binafsi ikiwemo nauli ya kwenda na kurudi nyumbani wakati wa likizo.
x) Aje na result slip ya O-level
xi) Aje na Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
xii) Viatu vya wazi (Sandles)
xiii) Tranka 01
xiv) Taulo .

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

- Shule hii inaendeshwa kwa mujibu na kanuni za Elimu ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara zenye dhamana ya Elimu nchini.
- Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo :-

i) Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima ,mtiifu na mwenye adabu wakati wote kwa walimu na wafanyakazi wasio walimu, wazazi, viongozi mbalimbali . ukaidi na dharau kwa viongozi ni marufuku.
ii) Mwanafunzi unatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule muda wote wa shule (Darasani) isipokuwa muda wa kazi za nje na michezo (utavaa nguo za michezo au shamba dress).
iii) Mwanafunzi ni lazima uwahi popote unapotakiwa na kwa wakati uliowekwa.
iv) Mwanafunzi ni lazima aheshimu kazi za darasani na nje na kuzifanya vizuri. Ni lazima kufanya mazoezi/ mitihani yote inayotolewa darasani.
v) Lugha chafu, matusi, ugomvi, fitina na kupigana kwa mwanafunzi ni mwiko kabisa.
vi) Unywaji wa pombe, uvutaji wa aina yoyote ya sigara au madawa ya kulevya ni mwiko kwa mwanafunzi

vii) Wizi ni marufuku na ni kosa kubwa kwa mwanafunzi
viii)Uharibifu na upotevu wa mali binafsi au ya umma ni kosa.
ix)Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa
akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufuku kuwa na mahusiano ya mapenzi awapo shuleni. Akibainika atafukuzwa shule.
x) SIMU HAZIRUHUSIWI KABISA SHULENI

**4.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

- Wizi
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 mfululizo bila taarifa /utoro
- Kugoma / kuhamasisha mgomo
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kw aujumla
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi , kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
- Kufuga ndevu.
- Ulevi au unywajiwapombenamatumiziyamadawayakulevya
- Uvutaji wa sigara
- Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- Kusababisha mimba au kupata mimba
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- Kudharau bendera ya Taifa
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

…………………………………………………

**PETER JOHN MBATA**
**MKUU WA SHULE**

## 02. FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANFUNZI /MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

……………………………….

………………………………

………………………………

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126.

MAFINGA

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE ILIYOKO MAFINGA- MKOA WA IRINGA

Mimi mwanafunzi............................................. Kidato cha .................. Mwaka....................

1. Nilizaliwa mnamo mwaka (Taja tarehe, mwezi na mwaka)..................... kijiji/Mjini...................

   Nimesoma shule ya sekondari ya ..................................... Wilaya ya...............Mkoa wa ....................

   - Nilikuwa kiongozi wa ..................................................................
   - Sikuwa kiongozi...........................................................
   - Michezo niipendayo ni ...................................................................
   - Nina kipaji cha.......................................................
   - Mengineyo Niwezayo..........................................................

2. Naahidi kuwa mtiifu wa sheria za shule, kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai, dharau kwa walimu, dharau kwa viongozi wa ngazi zote au wowote wale. Nitakuwa na nidhamu ya kujituma, kusoma kwa bidii na kwa mfano bora kwa wanafunzi wengine.

   Tofauti na haya niondolewe shuleni mara moja.

   Jina la mwanafunzi........................................ sahihi................. kidato........................ tarehe ..............

FOMU NA. 3. FOMU YA MZAZI / MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA , KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE HALALI YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

…………………………………………

……………………………………….

……………………………………….

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126,

MAFINGA

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA MWANANGU NA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE ILIYOKO MAFINGA-MKOA WA IRINGA

MWANAFUNZI …………………………………………………………………

KIDATO CHA ……………………………………….. MWAKA…………………………

1. Mimi ……………………………………………………….
   Mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu. Nakiri kuwa nimeelewa maelekezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.
2. Nakubali mwanangu aendelee na masomo na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kwa wakati wake. Kama ilivyoagizwa katika maelekezo ya kujiunga na shule.
3. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ili kufikia malengo yake ya kujiunga na shule hii.
4. Naahidi kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo hapa shuleni.
5. JINA LA MZAZI / MLEZI ………………………………………………. SAHIHI……………………….
6. ANWANI YA MZAZI/MLEZI……………………………………….
7. NAMBA YA SIMU ………………………………….. TAREHE ……………………………

FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

FOMU NA. 01. (FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI)

SEHEMU A

SHULE YA SEKONDARI
CHANGARAWE,

S.L.P. 126,

MAFINGA

KUMB.NA.MTC/CHSS/JI/2022/F5/08 ..............................

MGANGA MKUU,

HOSPITALI YA SERIKALI YA

………………………………………………..

S.L.P…………………..

MAFINGA

YAH: FOMU YA KUPIMWA AFYA YA MWANAFUNZI

Somo la hapo juu lahusika.

Tafadhari tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu wa kidato cha TANO mwaka 2022; kwa gharama za mzazi/mlezi wake.

Ni muhimu apimwe ili kujua afya yake kabla ya kuripoti hapa shuleni na kuendelea na masomo.

Natanguliza shukrani

……………………………………

PETER JOHN MBATA

MKUU WA SHULE

FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

SEHEMU B

YAH: MWANAFUNZI………………………………………………………..........

WA KIDATO CHA........................ MWAKA ..................

Matokeo ya vipimo vya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu ni:-

………………………………………………………………………………………………………………………..........

………………………………………………………………………………………………………………………............

………………………………………………………………………………………………………………………..........

………………………………………………………………………………………………………………………..........

Nathibitisha kuwa ………………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………………………........

………………………………………………………………………………………………………………………..........

JINA LA MGANGA…………………………………………………….

CHEO……………………………

SAHIHI……………………………. MUHURI…………………………… TAREHE…………………